**MUHTASARI WA MSWADA WA SHERIA YA KUANZISHA MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO.**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa heshima naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Mswada wa Sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na kupambana na Dawa za Kulevya na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

## 2.0 MADHUMUNI

**Mheshimiwa Spika,**
Madhumuni ya kufuta sheria Nambari 9 ya 2009 ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya ni kutunga sheria mpya ya kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya itakayokuwa na uwezo wa kupeleleza, kukamata, kuchunguza na hatimae kupeleka Mahkamani mashauri yanayohusiana na dawa za kulevya pamoja na makosa mengine yanayofanana nayo.

## 3.0 HISTORIA

**Mheshimiwa Spika,**
Mswada huu unatokana na dhamira ya **Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi** ya kusimamia kwa vitendo ibara ya 196 (a - g) ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 -2025 kwa kuhakikisha kwamba Serikali ya Awamu ya nane inaimarisha mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya ambapo, ameamuwa kuibadilisha Taasisi inayoshughulikia Dawa hizo kutoka Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya na kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya itayokuwa na uwezo kamili wa kisheria wa kukabiliana kikamilifu na uhalifu huu wa Dawa za Kulevya nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Sheria ya mwanzo ya kukabiliana na Dawa za Kulevya kwa Zanzibar ilitungwa mwaka 1915 ambayo ikijulikana kama '*the Abuse of Opiates Decree NO 5 of 1915'.* Kutokana na changamoto mbali mbali zilizojitokeza katika kukabiliana na uhalifu huu wa Dawa za Kulevya, Sheria hiyo ilifutwa na kutungwa Sheria mpya Namba 11 ya 1927 iliyojulikana kama '*the Dangerous Drugs Decree'*, ambayo baadae ilijulikana kama CAP 76 ya mwaka 1959, Sheria za Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**
CAP ya 76 iliendelea kutumika hata baada ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964 baadae mwaka 1986 CAP 76 ilifutwa na kutungwa Sheria mpya iliyojulikana kama '*the Pharmaceuticals and Dangerous drugs* Act no 6 of 1986'.

**Mheshimiwa Spika,**
Katika kuimarisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini, mwaka 1996 Serikali iliamua kuchukua hatua za kufuatilia na kupinga matumizi ya dawa za kulevya Zanzibar kwa kuanzisha Idara Maalumu ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya iliyokuwa chini ya Ofisi ya Waziri Kiongozi. Novemba mwaka 2000, Idara hiyo ilihamishiwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na kupewa majukumu ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya pamoja na Kinga na Tiba kwa walioathirika na matumizi ya dawa hizo.

**Mheshimiwa Spika,**
Mwaka 2003, Serikali iliendelea kuongeza nguvu katika mapambano kwenye usafirishaji na uingizaji wa dawa za kulevya kwa kupitisha Sheria ya Dawa na Kinga ya Usafirishaji wa Dawa za Kulevya Nam. 16/2003 "the drugs and prevention of Illicit Traffic Drugs Act.". Kutokana na kuwepo kwa sheria hiyo, mwaka 2004 Serikali ilifanya mabadiliko ya jina la Idara na kuitwa Idara ya Kupambana na Dawa za Kulevya na Kurekebisha Tabia. Katika utekelezaji wa Sheria hiyo, kasoro mbali mbali zilibainika na kupelekea Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia hili Baraza lako tukufu la kutunga sheria, lilitunga sheria mpya ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Nam. 9/2009 "the Drugs and Prevention of Illicit Traffic Drugs Act" ili kuimarisha mapambano zaidi. Sheria hii ndio inayotumika hadi sasa na ndio sheria iliyoanzisha Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Tume imepewa jukumu la Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya nchini pamoja na masuala mengine yanayofanana nayo. Katika kuitekeleza Sheria hii pamoja na mabadiliko ya namna ya kukabiliana na uhalifu wa Dawa za Kulevya, mapungufu mbali mbali ya kisheria yamekuwa yakijitokeza na kuipelekea sheria hiyo kufanyiwa marekebisho makubwa ya mara kwa mara kwa lengo la kwenda sambamba na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia pamoja na mbinu mpya zinazoibuliwa na wahalifu wa Dawa za Kulevya duniani siku hadi siku.

**Mheshimiwa Spika,**

Sheria hii Namba 9 ya 2009 imeipa taasisi (Tume) uwezo wa kuratibu tu masuala ya kudhibiti Dawa za Kulevya, Kemikali Bashrifu, Dawa tiba zinazodhibitiwa kisheria pamoja na makosa mengine yanayofanana nayo.

**Mheshimiwa Spika,**

Hivyo, basi Mswada huu wa sheria unaopendekezwa na Serikali katika Baraza lako Tukufu utapelekea kuongeza ufanisi katika kupambana na uhalifu wa Dawa za Kulevya nchini, ugeuzaji wa kemikali bashrifu pamoja na udhibiti wa dawa tiba.

## 4.0 MANTIKI

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kukabiliana na janga hili thakili linaloharibu nguvu kazi na uchumi wa nchi yetu, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **DKT. HUSSEIN MWINYI** katika taarifa aliyoitoa kwenye mazungumzo yake na kituo cha AZAM TV pale alipotimiza siku zake 100 za uongozi aliazimia kwa makusudi na kwa mustakbali mwema wa nchi yetu, kufanya mabadiliko makubwa kwenye tasnia ya kudhibiti dawa za kulevya, ikiwemo kuifuta Sheria ya Udhibiti na Usafirishaji wa Dawa za Kulevya, Nam. 9 ya mwaka 2009 na kutunga Sheria mpya inayoendana na kasi ya sasa ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya pamoja na Kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, yenye uwezo kamili wa kukabiliana na uhalifu huu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kama nilivyoeleza hapo awali kwamba ukuaji wa sayansi na teknolojia unaotokea ulimwenguni kwa sasa unatoa fursa pia kwa wahalifu wa dawa za kulevya kuwa na mbinu thabiti za kujikinga na hatua zinazoweza kuchukuliwa dhidi yao. Maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano ya kimtandao yanatumiwa na wahalifu wa dawa za kulevya na hivyo kupelekea jitihada zilizopangwa kufanywa na mtandao wa taasisi za kudhibiti Dawa za Kulevya kuingiliwa na kuharibu ushahidi. Pamoja na kwamba shughuli za utalii zina mchango mkubwa katika uchumi wetu, imeonekana kuwa kutokuwa na udhibiti imara katika sekta hiyo, kunapelekea ongezeko la uingizwaji na biashara ya dawa za kulevya nchini. Ukweli huu unalazimisha kuwepo na chombo imara na thabiti cha kusimamia udhibiti wa dawa za kulevya.

**Mheshimiwa Spika,**

Kuwa na Mamlaka kutasaidia kuweka misingi madhubuti ya usimamizi. Aidha, kwa kuwa eneo letu la mwambao wa Afrika ya Mashariki ni mojawapo ya njia kuu za biashara ya dawa za kulevya, kuwa na mamlaka kutaongeza fursa ya kushirikiana na mamlaka nyingine za kikanda na kimataifa zenye majukumu yanayofanana katika kudhibiti biashara na utumiaji wa dawa za kulevya**.**

Mamlaka itakayoanzishwa itakuwa ni chombo kinachojitegemea chenye uwezo wa kushitaki na kushitakiwa na kitakuwa kimejumuisha mambo yote yanayohusiana na chombo chenye kujitegemea.

## 5.0 UMUHIMU WA MSWADA HUU WA SHERIA

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa ujumla Mswada huu wa Sheria utapelekea kuwepo kwa Mamlaka yenye nguvu ya kisheria na thabiti ya kusimamia udhibiti wa dawa za kulevya nchini ambapo, faida nyingi zitapatikana kama ifuatavyo: -

1. Taasisi itakayoundwa itakuwa na uwezo wa kuchunguza, kukamata, kupeleleza na kufungua mashtaka mahakamani;
2. Kutakuwa na usimamizi madhubuti katika kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya;

3. Kutunza wenyewe vielelezo vya Dawa za Kulevya na kuepuka vielelezo hivyo kurudi kwenye jamii baada ya kesi ya msingi kumalizika;
4. Kupungua kwa kiasi kikubwa makosa yanayohusiana na utumiaji na usafirishaji wa dawa za kulevya, hali itakayopelekea kupunguza athari zitokanazo na dawa za kulevya;
5. Kuimarika kwa nguvu kazi hasa vijana na hatimaye kukuza uchumi wa nchi; na
6. Kudhibiti matumizi ya dawa zinazotumika kwa matibabu ambazo zinaweza kutumika kama dawa za kulevya.

## 6.0 MAMBO MUHIMU YALIYOZINGATIWA KATIKA RASIMU YA MSWADA WA SHERIA INAYOKUSUDIWA KUTUNGWA

**Mheshimiwa Spika,**

Mswada huu wa Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, umegawika katika sehemu kuu nane (08) na kujumuisha vifungu 86 vilivyozingatia masharti mbali mbali yanayohusiana na udhibiti wa matumizi na biashara ya dawa za kulevya, kati ya hivyo vifungu 26 ni makatazo juu ya mambo mbali mbali yanayohusu uhalifu wa dawa za kulevya na makosa yanayo fanana nayo kama ifuatavyo: -

**SEHEMU YA KWANZA (kifungu cha 1 hadi 2)**
Sehemu hii inaelezea Masharti ya awali ambayo yanajumuisha jina la sheria, kuanza kutumika na ufafanuzi wa maneno.

**SEHEMU YA PILI (kifungu cha 3 hadi 14)**
Sehemu hii inaelezea uanzishwaji wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar, Uwezo wa Mamlaka, Uwezo wa Kamishna Mkuu, Kazi za Mamlaka, Uteuzi wa Kamishna Mkuu, Sifa za Kamishna Mkuu, Kazi za Kamishna Mkuu, Wafanyakazi wa Mamlaka, Wajibu wa kula kiapo cha utiifu kwa wafanyakazi wa Mamlaka, Uwasilishaji wa Ripoti ya hali ya dawa za kulevya, Wajibu wa Serikali katika kuzuia dawa za kulevya, Kamati za mikoa na Kazi za Kamati za Mikoa.

**SEHEMU YA TATU (Kifungu cha 15)**

**Mheshimiwa Spika,**

Sehemu hii inaelezea kuanzishwa kwa Baraza la Taifa la Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Muundo, Uwezo na Majukumu ya Baraza.

**Baraza litajumuisha wajumbe wafuatao: -**

(a) Rais, ambae atakuwa Mwenyekiti;
(b) Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
(c) Waziri mwenye dhamana ya kudhibiti dawa za kulevya;
(d) Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais;
(e) Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais;
(f) Waziri anaeshughulikia mambo ya Sheria;
(g) Waziri anaeshughulikia Tawala za Mikoa;
(h) Waziri anaeshughulikia Afya na Ustawi wa Jamii;
(i) Waziri anaeshughulikia Vijana;
(j) Waziri anaeshughulikia Fedha;
(k) Mkurugenzi wa Mashtaka.

Rais anaweza kukasimu madaraka yake ya Uenyekiti kwa kumteua mtu mwengine kuliongoza Baraza.

Kamishna Mkuu atakuwa Katibu wa Baraza na atakuwa na jukumu la utekelezaji wa maamuzi ya Baraza.

**SEHEMU YA NNE (Kifungu cha 16 hadi 18)**

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii inahusiana na pendekezo la kuanzishwa kwa Mfuko, Usimamizi wa Mfuko na Hesabu na ukaguzi wa Mfuko.

**SEHEMU YA TANO (Kifungu cha 19 hadi 40)**

**Mheshimiwa Spika,**

Sehemu hii inaelezea makatazo ya kujihusisha na matumizi na biashara ya dawa za kulevya.

Sheria inakataza mambo mbali mbali sambamba na kuweka adhabu kali kama ifuatavyo: -

a. Kulima bangi, mirungi, kumiliki, kusafirisha, kuuza na kununua mbegu zinazoweza kuzalisha dawa za kulevya na adhabu yake ni kifungo cha maisha.

b. Kufadhili biashara ya dawa za kulevya (kif. 30) ambapo adhabu ya kosa hili ni kifungo cha maisha na kutaifisha mali zote zilizotokana na chumo la shughuli hiyo.

c. Kusafirisha dawa za kulevya, kujihusisha kwa namna yoyote kinyume cha Sheria na kemikali zinazoweza kuzalisha dawa za kulevya ambapo adhabu inayopendekezwa ni kifungo cha maisha kwa dawa za kulevya, kiwango (heroini na cocaine zenye uzito wa gramu zisizopungua 50, Kemikali bashirifu zisizopungua ujazo wa lita 50 au uzito wa gramu 50; kwa bangi na mirungi uzito usiopungua gramu 50) na chini ya kiwango hicho adhabu ni faini isiyopungua shilingi milioni hamsini au kifungo cha miaka 30 au zote kwa pamoja.

d. Kumiliki mashine, vifaa na maabara kwa lengo la kutengeneza dawa za kulevya, adhabu ni kifungo cha maisha na kutaifisha vifaa vyote, eneo pamoja na mali za wahusika.

e. Mmiliki wa jengo kuruhusu jengo litumike kwa dawa za kulevya (kif.24) atatozwa faini isiyopungua milioni 10 au kifungo kisichopungua miaka 15 na kisichozidi miaka 30 au adhabu zote mbili.

**Mheshimiwa Spika,**

f. Sheria hii vile vile inatoa adhabu kwa mtu yoyote atakaekataa kutoa taarifa ama ushahidi unaohusiana na uhalifu wa dawa za kulevya au kutoa taarifa za uongo na adhabu yake ni kutoa faini isiyopungua shilingi milioni 30 na isiyozidi shilingi milioni 50 au kifungo kisichopungua miaka 15 na kisichozidi miaka 30 au adhabu zote mbili.

g. Sheria inakataza kwa namna yoyote ile kusaidia au kusababisha kutendeka au kutenda uhalifu wa dawa za kulevya (kif. 32) na kutoa adhabu sawa sawa na mtenda kosa mwenyewe.

h. Sheria inakataza mtu yeyote kupanga au kushiriki katika kupanga kosa la dawa za kulevya (kif.33) na kuweka adhabu sawa na mtu aliyetenda kosa hata kama kosa lenyewe halikutendeka.

i. Sheria inatoa wajibu kwa mmiliki wa ardhi kutoa taarifa kwa Kamishna Jenerali kuhusu mazao haramu yaliyolimwa katika ardhi yake au shughuli yoyote haramu inayofanyika katika ardhi yake (kif. 54). Adhabu ni faini isiyopungua shilingi

milioni 10 na isiyozidi shilingi milioni 50 au kifungo kisichopungua miaka 15 na kisichozidi miaka 30 au adhabu zote mbili.

j. Sheria inakataza mtu yeyote kuwa na mali zinazohusishwa au zinazotokana na chumo la uhalifu wa dawa za kulevya (kif.70) na ikithibitika fedha au chumo hilo litataifishwa.

k. Sheria inamkataza afisa yeyote kumtaja/kumfichua aliyempatia taarifa za uhalifu wa dawa za kulevya (kif.44) na akifanya hivyo adhabu ni faini isiyozidi Milioni 15 au kifungo kisichopungua miaka 10 au vyote kwa pamoja.

**Makosa yasio na dhamana**

**Mheshimiwa Spika,**

l. Sheria hii inakataza Ofisa wa Polisi, Hakimu au mtu yoyote aliyeidhinishwa kutoa dhamana kwa makosa yote ya Dawa za Kulevya yaliyomo katika vifungu vifuatavyo: 21, 22, 26, 28, 30, 31, 32 au 34.

**Kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya**

**Mheshimiwa Spika,**

m. Ni kosa kukutwa na kiwango kidogo cha dawa za kulevya kwa matumizi binafsi. Adhabu ni faini isiyopungua shilingi milioni 3 na isiyozidi milioni 5 au kifungo kisichopungua mwaka 1 jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.

n. Sheria inaipa uwezo serikali kuanzisha Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia kwa ajili ya kuwatambua, kuwatibu, kuwarekebisha tabia na kuwarejesha katika jamii watumiaji wa dawa za kulevya.

**Sheria imekipa mamlaka yafuatayo chombo kinachoundwa**

**Mheshimiwa Spika,**

o. Kuratibu shughuli zinazofanywa na wadau za kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya;

p. Kutoa elimu kwa umma juu ya madhara ya dawa za kulevya;

q. Kuziwezesha taasisi za kiraia zikiwemo taasisi za nje zinazotoa elimu juu ya madhara ya dawa za kulevya;

r. Kuandaa miongozo mbali mbali inayohusu dawa za kulevya pamoja na madhara yake kwa jamii ikiwemo ya uanzishwaji wa nyumba za upataji nafuu (Sober Houses) na ya uelimishaji juu ya madhara ya dawa za kulevya;

s. Kuhamasisha jamii kushiriki katika kudhibiti matumizi na biashara ya dawa za kulevya; na

t. Kuhamasisha na kuhakikisha ushirikiano na jamii ya kimataifa katika kudhibiti dawa za kulevya.

**Mheshimiwa Spika,**

u. **Aidha,** Sheria hii inakataza kutumia dawa za kulevya kwa namna yoyote ile (Kif.23), adhabu ni faini isiyozidi milioni 5 au kifungo cha mwaka 1 au adhabu zote mbili.

v. Pia ni kosa kukutwa katika eneo ambalo hutumiwa na watumiaji wa dawa za kulevya.

w. Vile vile, ni kosa kukutwa na vifaa vinavyosadikiwa kuwa vimetumika kwa matumiz dawa za kulevya kama vile sindano.

**SEHEMU YA SITA (Kifungu cha 41 hadi 65)**

**Mheshimiwa Spika,**

Sehemu inahusiana na uwezo wa kufanya ukaguzi, upekuzi, kuzuia, kukamata, kuweka kizuizini na kuchunguza, Utumiaji wa uwezo bila ya kibali, Ufichaji wa dawa za kulevya ndani ya mwili, Utaratibu wa kutoa Zawadi, Kumlinda mtoa taarifa, Taratibu za ukamataji, Taratibu za upelelezi, Taratibu za upekuzi, Taratibu za kuchukuwa maelezo, Taratibu za kuzuia, Ukamataji na uzuiaji kutolewa taarifa ndani ya saa arubaini na nane, Ofisa aliyeidhinishwa kusimamia vitu vilivyokamatwa, kufanya uvamizi, Wajibu wa kutoa taarifa ya mazao yaliyolimwa, yaliyozalishwa au yaliyotengenezwa isivyo halali, Uwezo wa kushikilia mazao yaliyolimwa au kuzalishwa isivyo halali, Mamlaka kuteketeza dawa za kulevya, Mazingira yanayowezesha kukubalika kwa maelezo katika hali fulani, Haki ya kumiliki na kutumia silaha za moto, Wajibu wa maofisa mbali mbali kusaidiana, Kutoa taarifa za uongo kwa nia ovu, Adhabu dhidi ya ofisa

anayekataa kutimiza majukumu yake au kusaidia wahalifu, Nyaraka katika baadhi ya kesi, Uwezo wa kupata taarifa, Taarifa za mchunguzi wa Serikali na Maabara ya sayansi jinai.

**SEHEMU YA SABA (Kifungu 66 hadi 75)**

**Mheshimiwa Spika,**
Sehemu hii inahusiana na ufilisi wa mali, Utaifishaji wa mali, Ufilisi na utaifishaji wa mali ya mtu aliyetiwa hatiani nje ya Zanzibar, Uwezo wa kutaifisha mali au kitu kilichohusiana na kosa, Katazo la kumiliki mali iliyopatikana isivyo halali, Uwezo wa kufanya upelelezi au ukaguzi, Kuzuia akaunti ya benki, Tamko la Kamishna Mkuu kutaifisha mali, Uwezo wa kumiliki na Utaratibu wa ufuatiliaji na utambuzi wa mali.

**SEHEMU YA NANE (Kifungu cha 76 hadi 86)**

**Mheshimiwa Spika,**

Sehemu hii inazungumzia ufunguaji wa mashtaka ya makosa ya dawa za kulevya, Kinga dhidi ya hatua zinazochukuliwa kwa nia njema, Usafirishaji uliodhibitiwa kisheria, Rufaa dhidi ya uamuzi wa Kamishna Mkuu, Wajibu wa Serikali wa kuanzisha vituo vya tiba kwa watumiaji wa dawa za kulevya, Kukinga kutendeka kosa, kutunza amani, usalama na tabia njema, Uwezo wa Mamlaka kutoa maelekezo, utungaji wa Kanuni pamoja na Matumizi ya Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki (Usimamizi na Tozo) nam. 8 ya sheria za Jumuiya na Kufuta na kubakiza.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja.

………………………………………………

**DKT. SAADA MKUYA SALUM**

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS**

**ZANZIBAR**